





Wakala wa Vipimo Tanzania

JARIDA LA MWAKA 2015 - 2016 TOLEO LA KWANZA



YALIYOMO

1.	Dira /Dhima	2
2.	Utangulizi	3
3.	Historia ya Wakala.....	3
4.	Vipimo SACCOS.....	5
5.	Wakala wa Vipimo na Mkakati wa Kuongeza Viwanja vya Ofisi.....	5
6.	Elimu ya Matumizi Sahihi ya Vipimo kwa Wafanyabiashara na Viongozi wa Masoko.....	6
7.	Wakala Yashiriki katika Maonesho Mbalimbali kwa Ajili ya Kutangaza Huduma Zake kwa Wadau wa Ndani na Nje ya Nchi.....	8
	6.1 Matukio mbalimbali kwenye Maonesho ya Biashara Kitaifa.....	8
	6.2 Maonesho ya Milan 2015.....	9
	6.3 Maonesho ya Sido	11
8.	Taarifa Katika Mfumo wa Picha Zikionesha Mabaraza Mbalimbali ya Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo Wanayoyatumia Kuwasilisha Mawazo ya Watumishi wa Kada Zote Kada.....	13
9.	Baadhi ya Wafanyakazi Bora kwa Mwaka wa Fedha 2014/15.....	20
10.	Kanuni ya Kusimamia Uuzaji wa Gesi Aina ya LPG.....	24
11.	Ufungashaji Batili na Matumizi ya Vipimo Batili Jinsi Unavyodidimiza Uchumi wa Watanzania na Taifa kwa Ujumla.....	24
12.	Wakala wa Vipimo inavyotumia mifumo Mbalimbali kwa Ajili ya Kuboresha Ufanisi wa Utendaji Kazi.....	27
	12.1 Mfumo wa Clock In/Out.....	27
	12.2 Mfumo wa Task Management.....	28
	12.3 Mfumo wa Kielektroniki wa Cercivas.....	28
	12.4 Mfumo wa SHAKIRA.....	29
	12.5 Mfumo wa Kielektroniki wa Kukagua Bidhaa zilizofungashwa (Prepackages Inspection Soft Ware).....	30
	12.6 Mfumo wa Car Tracking.....	31
	12.7 Mfumo wa Epicor (Ver. 9).....	31
	12.8 HCMIS (Human Capital Management Information System).....	31

DIRA

DIRA

**Kufikia viwango vya kimataifa
katika utoaji huduma kwa
jamii kupitia matumizi sahihi
ya vipimo.**

DHIMA

DHIMA

**Kuthibiti vipimo vyote
vinavyotumika na
vinavyokusudiwa kutumika
katika sekta ya Biashara,
Mazingira, Afya na Usalama
na kuelimisha umma kuhusu
masuala ya vipimo nchini kwa
lengo la kumlinda mlaji.**

AFISA MTENDAJI MKUU NA UJIO MPYA WA MIAKA MITANO

2. Utangulizi

Wakala wa Vipimo (WMA) ilianzishwa tarehe 13 Mei, 2002 kwa Tangazo la Serikali namba 194 la tarehe 17 Mei, 2002. Ambapo hapo awali, kilikuwa Kitengo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na iliongozwa na viongozi mbalimbali.

Miongoni mwa majukumu ya Wakala wa Vipimo ni kuilinda jamii kutokana na madhara yatokanayo na matumizi mabaya ya vipimo katika sekta za Biashara, Afya, Usalama na Mazingira, kuthibiti ufungashaji wa bidhaa, kuwa kiungo kati ya taifa letu na taasisi mbali mbali za kikanda na kimataifa katika masuala ya vipimo, kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala ya Vipimo kwa wadau na kuhakikisha vifaa vyote vitumikavyo nchini kama standards za vipimo vinaulinganisho sahihi na ule wa kimataifa.

3. Historia ya Wakala




Kamishina wa Vipimo kabla na baada ya uhuru wa nchi hii

Mwaka 1960 – 1963
Idara ya vipimo ilikuwa chini ya Mrakibu wa Polisi ikiongozwa na Chief Inspector Mr. Hewitt chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani.



Kamishina wa Vipimo wa kwanza Mzalendo

Mwaka 1964 - 1984
Idara ya Vipimo ilikuwa chini ya Wizara ya Biashara na Ushirika na baadae kuwekwa chini ya Wizara ya Viwandana Biashara ikiongozwa na Michael Kabalo ambaye alikuwa ni Kamishina wa Vipimo.



Kamishina wa Vipimo na Afisa Mtendaji Mkuu wa kwanza wa Wakala wa Vipimo

Mwaka 1984 – 2008
Idara ya Vipimo iliongozwa na H. M. Tukai ambaye alikuwa ni Kamishina na Afisa Mtendaji Mkuu wa kwanza wa Wakala wa Vipimo.



Afisa Mtendaji Mkuu Wakala wa Vipimo

Kuanzia mwaka 2008 – 2015 WMA imekuwa ikiongozwa na Magdalena P. Chuwa ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu na Kamishina wa Vipimo nchini.

Kutokana na utendaji wake bora Magdalena P. Chuwa ameteuliwa kuiongoza tena Wakala wa Vipimo kwa miaka mingine mitano kuanzia 2015 – 2020.

Katika kipindi chote cha uongozi wake (2008 – 2015), kulikuwa na mafanikio mbalimbali kama vile:

- * Kuongezeka kwa maeneo mapya ya kazi ambayo ni pamoja na ukaguzi wa malori ya mchanga, matanki makubwa yakuhifadhi mafuta ya juu na chini ya ardhi, ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa, ukaguzi wa mita za maji, n.k
- * Uthibiti wa upimaji wa mafuta yaingiayo nchini (in terms of quantity) kwa lengo la kusimamia haki ya kila mdau yakiwemo makampuni ya mafuta na Mamlaka ya Mapato.

Kuongezeka kwa ufanisi wa utendaji kazi kwa kutumia vifaa vyaa kisasa katika ukaguzi.

- * Ununuzi wa magari kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi, ambapo kwa sasa Wakala wa Vipimo ina jumla ya Magari 48.
- * Uelewa wa jamii juu ya masuala ya vipimo umeongezeka kwa kuitia vipindi nya TV, Radio na Magazeti.
- * Kukarabati ofisi mikoa ya Shinyanga na Morogoro, pamoja na kufanya maboresho ya Ofisi za Wakala wa Vipimo (Mkoa wa Rukwa, Mwanza, Kagera, Lindi, Ruvuma na Kigoma)
- * Ununuzi wa Viwanja kwa ajili ya Ujenzi wa Majengo ya Ofisi, kwa sasa Wakala wa Vipimo inamiliki jumla ya viwanja 21 ambavyo vipo katika kila mkoa ambapo kuna ofisi za Vipimo na kuna baadhi ya Mikoa ambayo ina viwanja zaidi ya kimoja kama vile Mara, Shinyanga na Pwani
- * Ongezeko la Watumishi kutoka Watumishi 193 hadi kufikia Watumishi 275
- * Matumizi ya Mifumo ya kompyuta imeongeza ufanisi wa utendaji kazi. Mifumo hiyo ni pamoja na mfumo wa “Clock-In and Out, HCMIS, EPICOR, Task Management System, SHAKIRA, Car tracking System”



Afisa Mtendaji Mkuu Bi. Magdalena P. Chuwa akiwasilisha mada katika Baraza la Wafanyakazi

4. Vipimo SACCOS

Wakala wa Vipimo inamiliki Saccos ambayo ilianzishwa tarehe 30/01/2008 ikiwa na wanachama waanzilishi 13, ambapo hadi leo hii imefikisha idadi ya wanachama 178 na kati yao waliokopa wanafikia idadi ya wanachama 130 ambao wananaufaika na uwepo wa Saccos hiyo.

Ili kuijunga na uanachama wa Saccos ya Wakala wa Vipimo inakupasa kufuata taratibu zifuatazo:

- a. Kutoa kiasi cha Tsh. 130,000/= ambapo elfu kumi (10,000/=) ikiwa ni ada ya kiingilio na Laki moja na Ishirini (120,000/=) ni fedha ya kununulia hisa kwenye Saccos hiyo,
- b. Mwanachama mpya inampasa kusubiri miezi 3 tokea kuijunga kwake kwenye Saccos kabla ya kuanza kuhudumiwa,
- c. Mwanachama mpya inampasa kwenye akaunti yake kuwa na robo tatu ya kiasi cha fedha anachotaka kukopa ili kukamilisha mchakato huo wa ukopaji.

Vile vile kunafaida kubwa ya kuwa mwanachama wa Vipimo Saccos kwani wanachama wanaweza kupata mikopo ya hadi kiasi cha Shilingi Millioni 15, pia mwanachama anakua na uwezo wa kuiwekea akiba ambayo itamsaidia pindi anapokuja kuchukua mkopo bila kusahau kuwa mikopo inawasaidia wanachama kuendesha biashara zao binafsi na kukamilisha mambo mbali mbali yanayo wakabili kimaisha.

Malalamiko yalikuwepo hapo awali ambayo yalikua yanatokana na uwepo wa riba kubwa ya mwaka ambapo ilikuwa ni 22%, lakini kwa sasa malalamiko hayo yamepungua kwani

riba imepunguzwa hadi kufikia 13% kwa mwaka ambayo vilevile imesababisha hali ya marejesho kuwa nzuri kwani wanachama wamekua wakirejesha marejesho yaokwawakati. Vilevile palipo na kitu kizuri daima changamoto nazo hazikosekaniki, na changamoto kubwa inayoikabili Vipimo Saccos ni kiasi cha marejesho yanayokusanywa kwa mwezi ni madogo kukidhi kiasi cha mikopo inayoombwa na wanachama hali ambayo inasababisha mwanachama mwingine anayetaka kukopa asubiri kwa muda mrefu ili kupata mkopo wake. Vipimo Saccos inawakaribisha watumishi wa Wakala wa Vipimo bila kujali wafanyakazi wa mkataba wa masharti ya muda au ajira ya kudumu kuja kuijunga na Vipimo Saccoss ili kuweza kuweka akiba na kukopa kwani akiba haiozi.

5. Wakala wa Vipimo na Mkakati wa Kuongeza Viwanja vya Ofisi

Wakala wa Vipimo inamiliki jumla ya viwanja 21 ambavyo vipo katika kila mkoa ambapo kuna ofisi za Vipimo na kuna baadhi ya Mikoa ambayo ina viwanja zaidi ya kimoja kama vile Mara, Shinyanga na Pwani, hii yote ni kutokana na mpangilio wa Wakala wa Vipimo. Viwanja hivyo vitatumika katika kujenga ofisiza Wakala wa Vipimo katika kila mkoa ikiwa pamoja na karakana (workshops) maabara zitakazotumika kuhakiki Vipimo mbali mbali vinavyotumiwa na maafisa vipimo, taasisi mbalimbali, Viwanda na wafanyakabiashara.

Vile vile Wakala wa Vipimo ina mpango wa kutumia baadhi ya viwanja hivyo kujenga vituo vya upimaji (Calibration bay) ambavyo vitajengwa kikanda na vitakua na nafasi kubwa ya kuweza kuhakiki magari mengi zaidi na kupunguza msongamano wa magari kama ilivyo katika kituo chetu cha

upimaji cha llala. Pia taratibu za kupata viwanja hivyo zimezingatia Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Sura ya 113 na marekebisho yake ya mara kwa mara pamoja na kanuni zake na Sheria ya usajili wa Ardhi Sura ya 334.

Pia kumekua na maendeleo mazuri ya uendelezaji wa viwanja hivyo, kwani hadi sasa viwanja 12 vimekwisha pata hati ya umiliki. Matarajio ya Wakala ni kuwa viwanja 6 kati ya viwanja 21 hadi kufikia mwezi wa 6 mwaka huu wa fedha vitakuwa vimewekewa alama ya kuvitambulisha kwa kutumia nguzo zitakazowekwa kwenye mipaka ya viwanja. Aidha, viwanja viwili vya Misugusugu Pwani na Moshi Kilimanjaro ujenziwaofisina vituoma alumvya upimaji (calibration bay) umekwishaanza.

Mchakato huu wa upatikanaji wa viwanja na umiliki wake umekua ukikabiliwa na changamoto kubwa kutoka kwenye ofisi za halmashauri za manispaa za mikoa mbali mbali kwani utaratibu wa upatikanaji wa viwanja unakua na milolongo mirefu na wanachelewesha pia taratibu za upatikanaji wa hati za viwanja kwa wakati. Pia kuna baadhi ya Halmashauri

kwa mfano ya Singida walileta makadilio ya awali ya malipo ya kiwanja ambacho Wakala wa Vipimo walikwisha kilipia na baada ya muda kilichukuliwa tena na manispaa na kupewa eneo jingine hali ambayo inasababisha usumbufu na ucheleweshwaji wa mipango iliyokuwa imewekwa na ofisi.

6. Elimu ya Matumizi Sahihi ya Vipimo kwa Wafanyabiashara na Viongozi wa Masoko

Katika kuhakikisha majukumu ya Wakala wa Vipimo yanatekelezwa kwa usahihi, Wakala wa Vipimo kupitia Sehemu ya Habari, Elimu na Mawasiliano, inatoa elimu juu ya matumizi sahihi ya vipimo na kushauri wafanyabiashara watumie mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo katika kuuza mazao yao. Kwa mwaka 2015/2016 Wakala wa Vipimo imetoa elimu katika masoko ya Mabibo na Tandale.

Ni matumaini yetu tutaendelea kutoa elimu zaidi kwa wafanyabiashara wa bidhaa mbalimbali wanaouza bidhaa zao kwa kutumia vipimo batili kama vile visado, bakuli, mafungu na gunia la lumbesa.




Meneja wa Wakala wa Vipimo Mkoa wa Kinondoni akihojiwa na waandishi wa habari mara baada ya kutoa elimu ya vipimo kwa wafanyabiashara na viongozi wa masoko

Lengo la Wakala wa Vipimo kutoa elimu ya vipimo ni kuhakikisha wafanyabiashara wote wa Tanzania wanatumia vipimo sahihi katika uuzaji wa mazao yao kwa kutumia mizani iliyohakikiwa na Wakala wa Vipimo ili mfanyabiashara aweze kupata faida stahiki na pia



Meneja Sehemu ya Upimaji Bw. Richard Kadege akielezea madhara ya vipimo batili kwa wafanyabiashara wa Soko la Mabibo

Pia, Wakala wa Vipimo imetoa elimu kwa wafanyabiashara wa masoko juu ya mambo ya kuzingatia wakati wa ufungashaji wa bidhaa zao, ili mfanyabiashara huyo awe na fursa ya kuingia katika soko la ushindani ndani na nje ya nchi kwa kutumia ufungashaji sahihi. Hii itawasaidia wafanyabiashara wa Tanzania kuinua viwango vyao kwenye ufungashaji wa bidhaa na kuweza kuuza bidhaa zao nje



ya nchi.

Kaimu Meneja Sehemu ya Elimu, Habari na Mawasiliano Bi. Irene John akitoa elimu katika Soko la Mabibo (Dar es Salaam)

7. Wakala Yashiriki katika Maonesho Mbalimbali kwa Ajili ya Kutangaza Huduma Zake kwa Wadau wa Ndani na Nje ya Nchi

7.1 Matukio mbalimbali kwenye Maonesho ya Biashara Kitaifa MAONESHO YA SABASABA 2015



Mwakilishi kutoka Ubalozi wa Marekani Bw. Robert J. Donovan akisaini kitabu cha wageni mara baada ya



kutembelea banda la Wakala wa Vipimo Afisa Vipimo akitoa elimu umma kupitia televisheni



Wakili Tenes Rwiza akifanya Uhakiki wa jiwe la mteja kwa kulinganisha na standard ya Wakala katika maonesho ya Kimataifa ya Sabasaba, 2015



Wananchi wakipata elimu kuhusu vigezo vya kuzingatia wakati wa ununuzi wa mtungi wa gesi kwenye maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, 2015



Baadhi ya Washiriki walioiwakilisha Wakala wa Vipimo



katika maonesho ya Kimataifa ya Sabasaba, 2015
Afisa vipimo akieleza namna udanganyifu unavyofanywa na wafanyabiashara katika vipimo vya urefu katika

maonesho ya sabasaba, 2015

7.2 Maonesho ya Milan 2015

Wakala wa Vipimo ni mionganini mwa Taasisi kumi na mbili (12) hapa nchini zilizowezza kushiriki katika maonesho ya Kimataifa (Expo Milan 2015) nchini Italia chini ya uratibu wa TanTrade iliyopo chini ya Wizara ya Viwanda na biashara.

Kila nchi ilipatiwa siku maalumu (National Day) ya kutangaza utamaduni na vivutio vya nchi yake. Tanzania ilikuwa imepangiwa siku ya tarehe 13/07/2015 na mgeni rasmi alikuwa Makamu wa kwanza wa Rais wa Zanzibari Maalim Seif Sharif Hamad. Viongozi wengine walikuwa ni Balozi wa Tanzania nchini Italia Dkt. James Msekela, viongozi toka Wizara ya Viwanda amba ni Maria Bilia Raphael ambaye ni Naibu Katibu Mkuu, Tutubi Deo John Mangazi ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Utawala toka Wizara ya Viwanda na Biashara, Odilo Joseph Majengo ambaye ni Mkurugenzi wa Masoko pamoja na Kokuhaisa Katwire Rwabizi ambaye ni Afisa Biashara. Wengine walioshiriki maonesho hayo ni baadhi ya wawakilishi toka Wakala wa Vipimo wakiongozwa na



Afisa Mtendaji Mkoo bi. Magdalena Chuwa.



Hii ni sura ya nje ya banda la Tanzania



Baadhi ya Mikutano iliyofanyika pamoja na wawekezaji wa sekta mbalimbali zikiwemo sekta za mafuta, viwanda pamoja na pembejeo za kilimo. Hapa Wakala wa Vipimo ilipata nafasi ya kuelezea masuala ya vipimo na umuhimu wake kwa wawekezaji, wawekezaji walihakikishiwa na Afisa Mtendaji Mkoo wa Wakala wa Vipimo kwamba wasihofu kuja kuwekeza Tanzania. Wawekezaji hawa waliliza maswali mengi na walifurahishwa na Utendaji wa taasisi mbalimbali na huku wakionyesha nia na shauku ya kuja



Wageni wa mataifa mbalimbali waliweza kutembelea banda la Tanzania na kujionea vivutio vya kutosha. Bendera ya Tanzania ikipeperushwa kwenye maonesho hayo kuashiria siku ya Tanzania (National Day), kuonesha utamaduni, biashara na fursa zinazopatikana Tanzania.



kuwekeza nchini Tanzania.

Maafisa toka Tanzania wakisikiliza kwa makini mada mbalimbali zilizotolewa na Watanzania akiwemo Balozi wa Tanzania nchini Italia Dr. James Msekela, Makamu wa kwanza wa Rais wa Zainzibar pamoja na Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko toka Zanzibar.



Afisa Vipimo Mkuu Bi. Zainabu Kafungo akihudumia wateja walitembelea banda la Tanzania.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Bi. Maria Bilia Raphael akibadilishana mawazo na Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo mara baada ya ufunguzi wa maonesho.

Faida ya Maonesho ya Expo kwa Tanzania Kupitia WMA

- Ni matarajio ya Wakala kuwa wawekezaji wengi watavutika kuja kuwekeza nchini kwa sababu walipata uhakika kuwa kuna chombo kama Wakala wa Vipimo chini ya ushirikiano wa karibu na shirika la vipimo duniani kina simamia usahihi wa vipimo katika biashara, hivyo kwa wale wawekezaji wanaotaka kuja kuwekeza kwenye Viwanda walipata imani hasa katika masuala ya vipimo.
- Wakala wa Vipimo imejifunza mengi toka kwa mataifa mengine mfn. Technolojia inayotumika katika kilimo na jinsi wanavyozingatia matumizi ya vipimo sahihi kuanzia kupanda hadi kuuza na kupata faida kubwa na ndiyo sababu kuu ya kupata maendeleohayo, kupitia mfano huo Wakala itautumia kuelimishia wakulima wa Tanzania umuhimu wa kuzingatia vipimo sahihi mfano tutakavyoshiriki maonesho ya wakulima tutatumia nchi ya Italia kutolea mifano wakulima walivyoendelea zaidi kupitia matumzi ya vipimo sahihi.

7.3 Maonesho ya Sido

Wakala wa Vipimo ilishiriki katika maonesho ya wajasiriamali wadogo yaliyoratibiwa na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) kuanzia tarehe 26/08-01/09/2015. Taasisi zilizoweza kushiriki chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni WMA, TBS na SIDO wenyewe kama waratibu wakuu. Baadhi ya mashirika ya Serikali yaliyoweza kushiriki ni TFDA. Wengine walioweza kushiriki maonesho hayo ni makampuni ya kibenki kama vile NMB, CRDB, Benki ya Posta pamoja na mashirika mengine yanayokopesha na kuwezesha wajasiriamali.



Mkuu wa Mkoa wa Singida Dr. Paseko Kone (katikati) akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja wa Wakala wa Vipimo Mkoa wa Singida Bw. Dunford Manzi (kushoto) juu ya umuhimu wa kutoa elimu kwa wafungashaji. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa SIDO.



Kaimu Meneja Sehemu ya Elimu, Habari na Mawasiliano Bi. Irene John akitoa elimu kwa wajasiriamali juu ya mambo ya kuzingatia katika ufungashaji wa Bidhaa



Mmoja wa wafungashaji wakubwa wanaomiliki viwanda vya mafuta Mkoani Singida akiuliza swali kwa maafisa wa Wakala wa Vipimo.



Wananchi wakipata elimu kuhusu utambuaji wa mizani na mawe yaliyo sahihi




Afisa Vipimo Bw. Daudi Kola akiieleza mambo ya kuzingatia kabla ya kununua mtungi wa gesi

8. Taarifa Katika Mfumo wa Picha Zikionesha Mabaraza Mbalimbali ya Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo Wanayoyatumia Kuwasilisha Mawazo ya Watumishi wa Kada Zote



Baraza la 13 la Wafanyakazi la Wakala wa Vipimo liliofanyikia Mkoani Morogoro



Baraza la 14 la Wafanyakazi la Wakala wa Vipimo liliofanyikia Mkoani Dar es Salaam katika hoteli ya Kunduchi



Baraza la 15 la Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo lililofanyikia Mkoani Dodoma



Baraza la 16 la Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo liliofanyikia Mkoani Tanga




Katika Baraza la 16 la Wafanyakazi Wakala wa Vipimo kwa mara ya kwanza ilizindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja ikiwa ni majawapo ya kuongeza uwazi na uwajibikaji katika Utendaji wao wa kazi wa kila siku



Meza kuu katika Kikao cha 16 Mkoani Tanga





Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara Bi. Maria Bilia akizindua Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa Wakala wa Vipimo. Kushoto ni Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Bw. Salim Mohammed Chima na kulia ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo Bi. Magadalena P. Chuwa

Baraza la 17 la Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo liliofanyikia Mkoani Pwani katika Wilaya ya Bagamoyo



Uongozi wa ngazi ya juu katika Baraza 17 la Wafanyakazi wa Wakala wa Vipimo



9. Baadhi ya Wafanyakazi Bora kwa Mwaka wa Fedha 2014/15



Krishna Mahamba (Afisa Vipimo Mwandamizi, Mkoa wa Kinondoni) akipokea cheti cha ufanyakazi bora toka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo Bi. Magdalena Chuwa, wa kwanza kulia ni Mwenyekiti wa Tughe, Bwa. Magesa Biyani (Afisa Vipimo Mwandamizi)



Joseph Nyaulingo (Mwasibu Msaidizi, Makao Makuu) akipokea cheti cha ufanyakazi bora toka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo Bi. Magdalena Chuwa, wa kwanza kulia ni Mwenyekiti wa Tughe, Bwa. Magesa Biyani (Afisa Vipimo Mwandamizi)



Matias Joseph (Afisa Vipimo Mkuu, Mkoa wa Mara) akipokea cheti cha ufanyakazi bora toka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo Bi. Magdalena Chuwa, wa kwanza kulia ni Mwenyekiti wa Tughe, Bwa. Magesa Biyani (Afisa Vipimo Mwandamizi)



Malaki Nyangasi (Afisa Vipimo I, Mkoa wa Ilala) akipokea cheti cha ufanyakazi bora toka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo Bi. Magdalena Chuwa, wa kwanza kulia ni Mwenyekiti wa Tughe, Bwa. Magesa Biyani (Afisa Vipimo Mwandamizi)



Renatus Mathayo (Afisa Vipimo II, Mkoa wa Arusha) akipokea cheti cha ufanyakazi bora toka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo Bi. Magdalena Chuwa



Issack Kachoma (Afisa uchumi, Kitengo cha Mipango, Makao Makuu) akipokea cheti cha ufanyakazi bora toka kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Vipimo Bi. Magdalena Chuwa, wa kwanza kulia ni Mwenyekiti wa Tughe, Bwa. Magesa Biyani (Afisa Vipimo Mwandamizi)

10. Kanuni ya Kusimamia Uuzaji wa Gesi Aina ya LPG

Pamoja na huduma mbalimbali zinazotolewa na Wakala wa Vipimo, pia tunapenda kuhabarisha umma wa watanzania kuwa Kanuni mpya itakayosimamia uuzaji wa Gesi aina ya LPG (Liquefied Petroleum Gas) iliyofungashwa kwenye mitungi maarufu kwa matumizi ya majumbani imekamilika.



Wadau wakiwa katika vikao vya pamoja vya kuboresha kanuni ya gesi aina ya LPG

a. Nini maana ya LPG na inatokana na nini

Liquefied Petroleum Gas (LPG) ni aina ya gesi inayotokana na bidhaa za petroli ambayo huagizwa toka nje ya nchi kupitia Makampuni yanayoagiza mafuta au bidhaa za petroli (petroleum products).

Husafirishwa kwa Meli na kupakuliwa kuitia mabomba maalum na hatimaye kuhifadhiwa katika matenki makubwa kabla ya kupakiwa/kujazwa kwenye mitungi midogo midogo yenyewe uzito tofauti tofauti tayari kusambazwa kwa watumiaji.

b. Kwa nini Serikali kupitia Wakala wa Vipimo imeona hitaji na umuhimu wa kuwepo kwa Kanuni hii sasa?

Ni ukweli usiopingika kuwa, hivi sasa nishati ya gesi imechukuwa nafasi kubwa sana katika jamii kwa matumizi ya kupikia majumbani kutokana na nishati nyingine kama kuni, mafuta ya taa na hata umeme kuwa na gharama za juu sana au upatikanaji wake kutokuwa wa uhakika.

Aidha, uhamasishaji wa matumizi ya Gesi hii, unakwenda sambamba na mkakati wa Serikali wa kudhibiti matumizi ya bidhaa za misitu kwa lengo la kulinda mazingira.

Kutokana na hali hiyo, gesi imekuwa biashara kubwa hapa nchini na hivyo kusababisha makampuni mengi hasa yale yanayosambaza nishati ya mafuta kuingia pia katika biashara ya gesi ya kupikia ili kukidhi mahitaji ya soko. Hali hii imesababisha hitaji kubwa la udhibiti wa haki na usawa katika biashara hiyo kwa sasa kuliko ilivyokuwa hapo awali.

c. Maelezo juu ya Kanuni mpya ya gesi aina ya LPG

Kanuni hii imekamilika baada ya kuwashirikisha wadau mbalimbali ambao kwa kupitia vikao kadhaa waliweza kutoa maoni yao na baadaye kufanyiwa kazi ipasavyo na Wakala wa Vipimo kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Katiba na Sheria.

Kanuni hiyo ilisainiwa na Waziri wa Viwanda na Biashara Mh. Dr. Abdallah Kigoda (Mb) na sasa tayari inatumika baada ya kutangazwa katika gazeti la Serikali Toleo Na. 222 la tarehe 19/07/2013.

Lengo kuula Kanuni hiyo nikuboresha

usimamiaji wa matumizi ya vipimo sahihi katika sekta ya gesi hususan gesi aina ya LPG ili kuleta usawa na haki katika biashara hiyo. Wahusika wakuu ni pamoja na watumiaji wa majumbani, mahotelini, mashulen, Wajazaji na wasambazaji na wadau wote ambao kwa namna moja au nyingine wanatumia Gesi hiyo.

Aidha, ili kufanikisha azma hiyo, Wakaguzi kutoka Wakala wa Vipimo watapita kila eneo la biashara hiyo, kukagua kama wafanyabiashara wanatumia mizani iliyothibitishwa na Wakala wa Vipimo kwa usahihi na kwamba kanuni zote zinazotakiwa kuwa zimezingatiwa katika ufungashaji wa bidhaa hiyo.



d. Faida ya Kanuni hiyo kwa Wananchi

- ✓ Kuhakikisha kwamba biashara hiyo inafanyika kwa haki na usawa.
- ✓ Kuhakikisha makampuni na wafanyabiashara wa bidhaa hiyo wanazingatia vipimo sahihi vinavyotumika.
- ✓ Vipimo sahihi ni vile ambavyo vinatumika katika mfumo wa kimataifa (SI units) ambavyo nchi yetu imeridhia na siyo vinginevyo.
- ✓ Kumpa mwananchi nguvu ya kisheria ya kutambua uzito wa mtungi ulio tupu (tare weight), uzito wa gesi peke yake (net weight) na uzito wa mtungi pamoja na gesi (gross weight), na kutoa taarifa anapo baini udanganyifu.
- ✓ Kuhakikisha kuwa mtungi uliobeba Gesi unayo maandishi (Label) yanayoonyesha utambulisho wa bidhaa hiyo, jina la kampuni inayosambaza, namba ya mtungi (serial number), uzito wa mtungi bila gesi, uzito wa gesi peke yake na uzito wa mtungi pamoja na gesi.
- ✓ Kuhakikisha kuwa wafanyabiashara wa Gesi iliyofungashwa kwenye mitungi wanayo mizani katika eneo la biashara kwa ajili ya kuhakikisha uzito wa bidhaa hiyo pindi mteja anapohitaji kufanya hivyo.

e. Wito kwa Watanzania wote

Wakala wa Vipimo inatoa rai kwa wale wote wanaonunua au kutumia gesi aina hii (LPG) wasisite kutoa taarifa kwa Ofisi za Wakala wa Vipimo zilizopo katika kila Mkoa wa Tanzania Bara, endapo watabaini vitendo ambavyo ni kinyume na matakwa ya Kanuni tajwa.

Kanuni hizo zinapatikana katika Ofisi zetu zote za Mikoa Tanzania Bara na kwamba Mameneja wetu wa Mikoa yote wapo tayari kuwashudumia.

Hivyo, wananchi watusaidie kutoa taarifa pale wanapohisi au kuona wafanyabiashara wasio waaminifu wanatumia vipimo pungufu au batili kwa kuwasiliana na ofisi zetu zilizopo kila mkoa.

11.Ufungashaji Batili na Matumizi ya Vipimo Batili Jinsi Unavyodidimiza Uchumi wa Watanzania na Taifa kwa Ujumla

a. Maana ya Ufungashaji na upimaji batili



Afisa Vipimo akitoa elimu kwa wafanyabiashara wanaotumia vipimo batili

b. Madhara yanayotokana na ufungashaji na matumizi ya vipimo batili yanababisha kudhoofisha uchumi wa Taifa kwa:-

Ufungashaji kinyume na Sheria ya Vipimo Sura 340, (iliyopitwa Mwaka 2002) pamoja na Kanuni zake.

- Kumpunja mkulima/ mfanyabiashara na mlaji/ mtumiaji
- Kuathiri afya za wabebaji - Nguvukazi ya Taifa (ubebaji wa lumbesa)
- Halmashauri kukusanya mapato pungufu wanapotoza ada kwa gunia badala ya uzito au ujazo.
- Kuathiri miundombinu- Barabara, Mabomba n.k.
- Kuharibika kwa haraka kwa vyombo vinavyosafirishia mazao
- Kuathiri maisha (uhai) na mali za wananchi
- Kuongeza walemavu, tegemezi na yatima
- Kuathirika kwa biashara ya kimataifa

c. Changamoto

- Uhaba wa rasilimali watu
- Kuwa na majukumu mengine (siyo tu kusimamia vipimo batili mf. Vituo vya mafuta, bidhaa zilizofungashwa, mabucha, n.k. vyote vinahakikiwa na Wakala wa Vipimo)
- Kuhatarisha maisha ya watumishi katika baadhi ya mikoa baada ya kuchukua sura ya kisiasa
- Kuachiwa Wakala wa Vipimo peke yake wakati ni suala mtambuka lenye kugharimu pesa nyangi

d. Ufumbuzi/Suluhi

- Ushirikiano kati ya WAKALA WA VIPIMO, TAMISEMI, KILIMO na wadau



Maafisa toka Wakala wa Vipimo wakitoa elimu katika soko la Mabibo juu ya madhara yanayotokana na matumizi ya vipimo batili

wengine wote zikiwemo ngazi mbalimbali za Serikali, Asasi za Kidini, Kisiasa, Kiraia, vyombo vya habari na wananchi kwa ujumla.

- Kuanzisha vituo vya kununulia mazao vijijiini (buying centres)
- Halmashauri kutunga Sheria ndogo (kanuni) za kukomesha ununuzi wa mazao mashambani.

e. Wito Wetu kwa Watanzania

Wakala wa Vipimo inasisitiza matumizi ya vipimo sahihi na ni kosa la jinai kwa mujibu wa sheria ya vipimo kutumia kipimo chochote ambacho hakijahakikiwa na Wakala wa Vipimo.

f. Maelezo Mengine ya Nyongeza



Afisa Vipimo Mkoo Bi. Zainabu Kafungo akitoa elimu ya matumizi sahihi ya vipimo kwa wakulima katika Mkoa wa Morogoro

- Baadhi ya Wafanyabiashara wanajipunja kwa kutokujua kwa kuwazidishia wateja wao na mwisho wa siku wanafilisika na kushindwa kurejesha mikopo hasa wamama.

Wakala wa Vipimo itaendelea kutoa elimu kwa wananchi ili wajue haki zao na madhara yanayotokana na matumizi ya vipimo batili.

- Wakala itaendelea kuwashauri wafanyabishara kuhusiana na vipimo vinavyositahili kutumika katika biashara.
- Wakala itaendelea kuwashauri serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza au kuondoa kabisa kodi zinazohusiana na vipimo zikiwemo mizani ili ziweze kununuliwa kwa bei nafuu na hivyo, kumwezesha mfanyabiashara kununua mizani hiyo kwa bei nafuu.
- Pia, Wakala wa Vipimo inaomba ushirikiano wa wadau wengine zikiwemo serikali za mitaa, taasisi za kidini, wanasiasa, vyombo vya habari, serikali za vijiji hadi taifa kukomesha matumizi ya vipimo batili.
- Ushauri: wafanyabiashara Watumie vipimo vilivyohakikiwa na Wakala wa Vipimo ili kutoa haki kwa pande zote (muuzaji na mnunuzi).

12. Wakala wa Vipimo inavyotumia mifumo Mbalimbali kwa ajili ya Kuboresha Ufanisi wa Utendaji Kazi

Wakala wa Vipimo pamoja na huduma zake nyingi inazotoa kwa umma wa watanzania, imendelea kubuni na kutumia mifumo mbalimbali kwa lengo la kuongeza ufanisi kazini. Mpaka sasa wakala inayo mifumo 8 ambayo ni:

Mfumo wa clock in and out, mfumo wa task management system, mfumo wa kielectroniki wa CERCIVAS, mfumo wa Shakira, mfumo wa kielektroniki wa kukagua bidhaa zilizofungashwa (prepackages inspection soft ware), mfumo wa Car Tracking, mfumo wa Epicor (Ves.9) pamoja na HCMIS (Human Capital Management Information System). Baadhi ya mifumo hii ni ile inayotumiwa Kitaifa na mingine (5) imebuniwa na watumishi ndani ya wakala.

12.1 Mfumo wa Clock In/Out

Ni mifumo wa mahudhurio kazini, wa kielektroniki unaomwezesha mwajiri akiwa mahali popote duniani ambapo pana mtandao kujua muda ambao mtumishi ameingia na kutoka ofisini kulingana na muda uliopangwa kisheria. Na kama mtumishi akichelewa kufika kazini au akiwahi kuondoka ofisini tofauti na muda uliopangwa ina mlazimu atoe sababu muhimu. Kumbukumbu zote zinahifadhiwa kielectroniki. Wakala ilianza rasmi kutumia mfumo huu kuanzia Julai 2013, kwa ofisi ya Makao Makuu Dar es Salaam, na hatimaye kwa ofisi zake zote Mikoani kuanzia Julai 2014.

Faida: (1) Inawasaidia viongozi (wakurugenzi, mameneja na wakuu wa vitengo) kokote walipo kuona mahudhurio ya watumishi wa ofisi zao na pia, inasaidia watumishi kuwahi ofisini na imesaidia kujenga nidhamu ya mahudhurio kazini kwa watumishi.

Kabla ya mfumo huu; (1) Watumishi walikuwa wanajiardikisha kwenye kitabu cha mahudhurio pekee ambapo ilikuwa haiwawezeshi

viongozi wa Wakala wa Vipimo kufahamu mahudhurio ya watumishi mikoani kote, pia walikuwa hawawezi kufahamu mahudhurio wakiwa nje ya vituo vyao vya kazi. (2) Ilikuwa si rahisi kujua muda kamili ambao mtumishi amefika, watumishi wengine ni wadanganyifu walikuwa hawaandiki muda kama walivyofika (3) Ilikuwa si rahisi kujua muda kamili ambao mtumishi ametoka ofisini, baadhi ya watumishi walikuwa hawajibiki ipasavyo na kuondoka kabla ya muda (huu tunaita wizi wa muda).

Changamoto: Mfumo huu ni wa kielektroniki unahitaji kuwa na mtandao wa kuaminika ili uweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Nini kifanyike: Wakala imejipanga kuhakikisha wana wataalam wa kutosha pamoja na vitendea kazi vya kuaminika ili kwenda sambamba na kasi ya maendeleo ya nchi.

12.2 Mfumo wa Task Management

Ni mfumo unaomwezesha kila kiongozi kutuma kazi zake za wiki pamoja na majukumu ya wale wote walio chini yake zinazoendana na mpango kazi wa mwaka (business plan) uliotengenezwa na Wakala wa Vipimo kutokana na mpango mkakati kwa kipindi cha miaka mitano (SP). Aidha mfumo huo ni "webbased", ambapo Afisa Mtendaji Mkoo au kiongozi wa Idara anaweza kufuatilia Utendaji wa watumishi walio chini yake akiwa nje ya kituo cha kazi (likizo, safari au Dharura yoyote), kupitia tovuti ya Wakala wa Vipimo (www.wma.go.tz) na hivyo, kuweza kutoa maelekezo katika kuboresha utendaji na hatimaye kupata matokeo tarajiwa kwa wakati.

Wakala ilianza kutumia mfumo huu Julai, 2012.

Faida: (1) Kila mtumishi anajua anatakiwa kufanya nini kwa siku, (2) Mfumo huu unamsaidia mtumishi kuyajua malengo yake ya wiki, mwezi, mwaka pamoja na mipango mikakati ya muda mrefu, (3) Kutambua mchango wake katika Wakala wa Vipimo kwa kukamilisha majukumu yake.

Kabla ya mfumo huu; (1) Watumishi walikuwa hawamalizi kazi kwa wakati (2) Baadhi ya watumishi kutojua anachotakiwa kufanya kwa siku/wiki husika (3) Pia, baadhi ya watumishi walikuwa wanashindwa kukamilisha majukumu kwa kutumia muda mwingi kufanya mambo yasiyokuwa na tija kwa ofisi.

Changamoto: (1) Mtumishi akipanga vibaya malengo yake kwa mwaka hujikuta hana kazi ya kufanya matokeo yake anafanya kazi katika wakati mgumu kwa kujilazimisha kutafuta majukumu ambayo hayako katika mpango wa wakala na matokeo yake kuona anaonewa au kunyanyaswa kwa kuulizwa mara kwa mara nini amefanya kwa kila wiki au kila mwezi.

Matarajio yetu ni kuendelea kuboresha mfumo huu hasa kwenye upangaji wa mipango ya Wakala na kuweza kuutumia kupima Utendaji kazi wa watumishi kupitia OPRAS.

12.3 Mfumo wa Kielektroniki wa Cercivas

CERCIVAS (Certificate of Correctness Issuance and Validation System)

ni mfumo ambao unawezesha utoaji wa hati ya usahihi wa kipimo na ufuatiliaji wake. Mfumo huu uliana kutumiwa mwaka

2008, kabla ya hapo Wakala wa Vipimo ilikuwa inatumia mfumo wa risiti (manual system).

Faida ya mfumo huu (1) Inaleta ufanisi katika kazi, mf. baada ya gari tu kupimwa mmiliki anapewa stika (coded sticker) maalum papo hapo na mtaalamu atakuwa tayari ana taarifa zote za mmiliki kwenye mfumo na akihitaji kujua kama gari bado lina cheti sahihi au imekwisha muda wake anaangalia kwenye mfumo na kupata taarifa zote kwa kutumia kifaa maalum kiitwacho scanner kinachowasiliana electronically na server ya WMA. Hivyo, Scanner hutumika kuhakiki taarifa mbalimbali zinazohusiana na upimaji wa Malori ya Mchanga na Kokoto pamoja na Malori yanayosafirisha mafuta. (2) Wateja wanahudumiwa kwa wakati (3) Usumbu na ubishani na wateja haupo tena, kwa kuwa afisa akitaka taarifa anaangalia tu kwenye mfumo kuititia kifaa hicho maalum.



Hili ni lori ambalo tayari limehakikiwa na Wakala wa Vipimo na kuwekewa alama.



Hili ni kifaa maalumu kinachosaidia kuhakiki usahihi ujazo wa Malori yabebayo mchanga

Kabla ya mfumo huu; hakukuwa na ufanisi mzuri wa kazi, (1) Ilikuwa inahitaji Afisa Vipimo kuchukuuwa muda mrefu kukagua gari (2) Pia,

mteja alikuwa anachelewa kupata taarifa na wengine walikuwa wanagushi yeti.

Changamoto: (1) Kutohaka na mabadiliko ya teknolojia inalazimika kutumia gharama kubwa katika ununuzi wa vifaa vipyta ili kuendana na kasi ya teknolojia hiyo.

Nini Kifanyike: Wakala wa Vipimo itaendelea kujitahidi kuendana na teknolojia ya sasa kwa kuongeza bajeti katika ununuzi wa vifaa vyta Kisasa.

12.4 Mfumo wa SHAKIRA

Ni spread sheet inayotumika kurahisisha uandaaji wa ripoti ya siku, wiki na mwezi, ambayo inaainisha idadi ya vipimo, aina ya vipimo na ada iliyokusanywa. Mfumo huu ulianza mwanzoni mwa mwaka 2009 ambapo ulikuwa unatumika katika Mkoa wa Temeke pekee, na mwishoni mwa mwaka 2010 mfumo huu ukaanza kutumika nchi nzima kwenye ofisi zote za Wakala wa Vipimo.

Faida:(1)Kuanzishwakwamfumo wa SHAKIRA kumerahisisha uandaaji wa taarifa za mwezi,



Afisa Vipimo akifanya Uhakiki wa Malori ya Mchanga na kokoto

hivyo, mtaalamu anaweza kuandaa taarifa ya siku/ mwezi kwa muda mfupi na kuendelea na majukumu mengine (2) Kufanya kazi kwa usahihi na kwa uaminifu (3) Mfumo wa SHAKIRA haumpi nafasi mtumiaji kugushi taarifa kwa kuwa mfumo tayari umekokotolewa na unazo "formula" maalum zinazomwezesha Meneja wa Mkao kujua idadi ya vipimo alivyotakiwa kuhakiki kwa eneo Fulani, vimebadilika kiasi gani na hata kiasi cha makusanyo ya uhakiki huo. (4) Pia, inarahisisha kulinganisha makadirio ya bajeti pamoja na halisia ambapo inamsaidia Afisa Vipimo kujua kama amefikia malengo aliyojiwekea kwa kipindi husika. Hali ya utendaji kazi kabla ya mfumo huu: Ilikuwa ni kazi kubwa kulinganisha uhalisia wa ripoti na bajeti kwa mwezi husika, pia muda mwingu ulikuwa ukitumika kuanzia wiki moja hadi tatu katika kukokotoa mahesabu na hivyo kupelekeea maafisa kutumia muda mrefu kuandaa ripoti za

mwezi.

Ila kwa sasa kwa kutumia mfumo wa SHAKIRA, kazi ya ukokotoaji wa mahesabu ya vipimo inafanyika ndani ya siku moja tu na taarifa ya mwezi inapatikana kwa wakati na kutumwa Makao Makuu kwa wakati.

Changamoto: (1) Watumiaji wa mfumo huu lazima wawe na ujuzi wa kutumia programu ya kompyuta ya "Excel" mfumo hauwezi kuhuisha taarifa za mwaka mzima (ku-update data).

12.5 Mfumo wa Kielektroniki wa Kukagua Bidhaa Zilizofungashwa (Prepackages Inspection Software)

Ni spread sheet inayotumika kutoa matokeo ya upimaji wa bidhaa zilizofungashwa moja kwa moja kwa usahihi, ikiwa imezingatia matakwa ya Shirika la Kimataifa la Vipimo (International Organization of Legal Metrology, (OIML). Mfumo huu ulianza mwaka 2011.

Faida: (1) Inarahisisha kutoa taarifa mapema (2) Mteja anapata matokeo mara tu baada ya kupimiwa bidhaa zake (3) Pia, kutokuwepo kwa makosa ya kimahesabu kwa kuwa kila data inayoingizwa katika kompyuta hufanyiwa mahesabu (4) Inaongeza kuaminiwa na mteja kwani kila kitu kinafanywa mbele ya mteja na huweza hata kushirikishwa kuchagua sampuli (sample) ya ukaguzi huo.

Kabla ya mfumo huu kuanza: (1) Ilikuwa inachukuwa muda mrefu mteja kupata matokeo ya upimaji (2) Pia, makosa ya

kimahesabu yalikuwa yanatokea kutohana na ukokotoaji wa calculator (manual calculation). Changamoto: (1) Utumiaji wa mfumo huu unahitaji mafunzo, hivyo tunaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi, ili waweze kwenda vizuri na mfumo (2) Umakini mkubwa unahitajika wakati wa kuingiza data za ukaguzi huo ili kupata matokeo sahihi na hatimaye mkaguzi kufanya uamuzi sahihi.

Matarajio: kuboresha zaidi na kuwa na mafunzo zaidi kwa watumishi ili waweze kutumia mfumo huu kwa ufanisi zaidi.

12.6 Mfumo wa Car Tracking

Ni mfumo unaowezesha kufuatilia na kupata taarifa mbalimbali za magari kwa kutumia njia ya kielektroniki, ambapo taarifa inapokelewa kwa kutumia simu ya mkononi au kompyuta. Wakala ilianza kutumia mfumo huu mwaka 2012.

Faida: (1) Unawezesha kujua gari liko wapi na kujua mwendo kasi wa gari unaotumika (2) Ulinzi, ikitokea gari limeibiwa kuna uwezekano wa kuangalia gari liko wapi na ukalizima (3) Pia, inasaidia kuzuia matumizi mabaya ya gari tofauti na matumizi ya ofisi, hivyo mwajiri hupata taarifa gari lilipo (4) Mwajiri na maafisa husika kuweza kufuatilia mienendo ya gari zote za Wakala wa Vipimo zilizofungwa mfumo huo wakiwa popote. (5) Imeleta nidhamu ya matumizi mazuri ya magari ya Wakala.

Kabla ya mfumo kuanza: (1) Magari yalikuwa yanachakaa kwa muda mfupi,

kwa kuwa madereva au maafisa husika walikuwa wanaenda kwa mwendo kasi na muda mwingine walikuwa wanaenda safari nyingine tofauti na za kiofisi (2) Pia, ajali zilikuwa nyingi kutohana na kuendesha gari kwa mwendo kasi

12.7 Mfumo wa Epicor (Ver. 9)

Ni mfumo wa kielektroniki wa kutunza na kutoa taarifa za kifedha (integrated financial management system). Mfumo huu uliana kutumika 2013, na huwezesha taratibu za malipo kufanyika kielektroniki hadi uandishi wa hundi.

Faida ya mfumo huu: (1) Uwajibikaji na uaminifu, kwa kutumia mfumo huu wa EPICOR, huwezi kutumia bajeti tofauti na mpangilio. (2) Kutoa Taarifa za kifedha kwa wakati.

Changamoto: Mfumo huu unatumika Makao Makuu pekee..

Nini Kifanyike: Kuna mpango wa kuunganisha hadi Mikoani kwa awamu ili kuleta ufanisi zaidi kwa kuwa taasisi imepata kibali cha kuajiri wahasibu wa kutosha kwa ofisi zake mikoa yote.

12.8 HCMIS (Human Capital Management Information System)

Ni mfumo unaohifadhi Taarifa za rasilimali watu na umeunganishwa na kompyuta za UTUMISHI na Wizara ya fedha. Hivyo, mara mtumishi anapoajiriwa, taarifa zake zote huingizwa katika mfumo huo. Na hata baadaye anapotakiwa kupandishwa cheo, idhini toka mamlaka kama UTUMISHI hutolewa kwa kuitia mfumo huo (electronically) na taratibu nyingine Kuendelea.

HITIMISHO

Kwa kutumia mifumo tajwa hapo juu mwajiri ameweza kuhakikisha masaa halali ya mtumishi kuwepo kazini yanafikiwa na yanatumika vizuri na katika kufanyakazi na kupata matokeo tarajiwa kwa wakati. Hivyo, kuchangia



Wakala wa Vipimo Tanzania